JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

SHULE YA SEKONDARI - MUBABA
S.L.P. 185 BIHARAMULO
KAGERA.
SIMU NAMBA: 0755-298 756
0758534860

MZAZI **/** MLEZI WA MWANAFUNZI
…….
S.L.P ……...
…….

YAH: <u>MA ELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MUBABA</u>
<u>KIDATO CHA TANO HALMASHAURI YA WILAYA YA BIHARAMULO,</u>
<u>MKOA WA KAGERA</u>

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka 2020. Tahasusi ya CBG/PCB/PCM. Shule ya Sekondari Mubaba ipo umbali wa kilometa **83** mashariki mwa mji wa Biharamulo na kilometa 131 magharibi mwa mji wa Kahama.Aidha shule hii ipo pembeni mwa barabara kuu itokayo Kahama kuelekea Ngara, kati ya miji midogo ya Runzewe na Nyakanazi. Ili uweze kufika kwa urahisi shuleni hapa kwa kutumia mabasi makubwa ya Abiria kutoka sehemu mbalimbali za Nchi itakubidi kushukia mji mdogo wa Runzewe kisha utachukua usafiri wa aina ya magari madogo ya abiria (Hiace) ama pikipiki (Bodaboda) kuelekea shuleni, kwa nauli ya Tshs. 3,000/= Muhula wa masomo unaanza mwezi Julai 2020. Hivyo Mwanafunzi unatakiwa kuripoti Shuleni tarehe tajwa,

2. Mambo muhimu ya kuzingatia

2.1. <u>Sare ya shule</u>

a) Kwa wasichana - Blauzi/ Mashati mawili meupe ya mikono mifupi yasiyo na urembo wowote.
   - Sketi mbili rangi nyeusi za kitambaa cha suruali / suti, zenye marinda manane ya kuzunguka kiuno, ndefu mpaka chini.

   Kwa wavulana - Mashati mawili meupe ya mikono mifupi
   - Suruali mbili rangi nyeusi zenye marinda mawili kila upande, zisiwe na mifuko ya kubandika nyuma au mbele, zisiwe za kubana maarufu kwa jina la (modal). Aidha hakikisha zinavaliwa kiunoni, pia ziwe na pindo chini miguuni, yaani (Turn-up)

b) Rangi ya hijab (kijuba) iwe nyeupe, na suruali yake nyeusi.

c) · Sare ya michezo kwa shule hii ni; T-shirt/Jezi mbili za rangi ya bluu, bukta/Track suit" mbili za rangi ya bluu, raba na soksi / stocking za michezo.

d) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi, viwe vya ngozi.
e) Soksi jozi mbili nyeupe.
f) Mkanda wa kuvalia suruali ni mweusi wa ngozi, usiwe na chuma kipana wala urembo wowote.
g) Sweta mbili : sare ya shule inapatikana hapa shuleni
h) Nguo za kushindia "T-shirt" Sare ya shule inapatikana hapa shuleni (kwa wavulana na wasichana).

Gauni (shamba dress) Sare ya shule lenye rangi ya pinki linapatikana hapa shuleni (kwa wasichana tu)

– Suruali mbili za rangi "damu ya mzee" yenye sifa kama kwenye kipenge1e (a) Hapo juu, (kwa wavulana tu)
i) Tai rangi nyeusi na nyeupe(wote wavulana na wasichana) zinapatikana shuleni.

2.2. <u>Ada na michango ya shule</u>

a. Ada ya shule kwa mwaka ni Tshs. 70,000/= (Shule hii ni ya bweni tu). Unaweza kulipa kiasi cha Tshs. 35,000/= kwa muhula au kulipa ada yote kwa mara moja. Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule Na. 31701200088 katika benki ya NMB (Tafadhali andika jina la mwanafunzi kwenye pay in slip).
b. Michango inayotakiwa kulipwa na wazazi ni;
   i. Shilingi 25,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani.
   ii. Shilingi 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha.
   iii. Shilling 20,000/= kwa ajili ya taaluma.
   iv. Shilingi 30,000/= kwa ajili ya kuwalipa wapishi na walinzi.
   v. Shilling 2,000/= nembo ya shule
   vi. Shilingi 10,000./= kwa ajili ya huduma ya kwanza kwa mwaka. Tunashauri kila Mwanafunzi aje na bima yake ya Afya ya NHIF.au 51, 000 ili atengenezewe bima ya NHIF
   vii. Shilling 20,000/= mitihani ya kujipima "Mock"
   viii. Fedha ya tahadhali Tshs. 5,000/= (haitarejeshwa).

c. Mahitaji muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuleta Shuleni:-

   i. Kiti na meza.
   ii. Ream ya karatasi 1 (kwa mwaka),
   iii. graph pad 1 (kwa mwaka)
   iv. Vitabu vya masomo husika kwa tahasusi yako
   v. "Dissecting kit" kwa wanafunzi wa "Biology"
   vi. "Scientific calculator"
   vii. Godoro la nchi 3/6 au 2 ½ /6
   viii. Mashuka pair 2, rangi ya "light blue", Blanketi 1, foronya 1, chandarua l rangi ya "lighrblue"
   ix. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kikombe na kijiko)
   x. Ndoo moja ya ujazo wa lita 20 au ndoo mbili za ujazo wa lita 10 ziwe na mifuniko tafadhali, Gereni/ chupa kubwa kwa ajili ya kujitunzia maji ya kunywa.

xi. Kwanja 1, jembe 1 na mpini wake, hard brush/mopper 1, panga 1, ufagio wa nje (chelewa) 1, ufagio wa ndani (soft bloom),

xii. Dawa ya chooni lita 5

xiii. Mwanafunzi anatakiwa aje na picha nne za wazazi, ndugu wa karibu wanao weza kumtembelea shuleni hapa .

N.B: VITU VIFUATAVYO VINAPATIKANA KWENYE DUKA LA SHULE KWA BEI NAFUU

- **Ream**
- **Graph pad**
- **Jempe na mpini**
- **Fyekeo**
- **Soft broom**
- **Panga**
- **Mopper**
- **Dawa ya chooni**
- **Godoro 3/6 na 2 ½/6**
- **Track suit (rangi ya blue)**
- **Scientific Calculator**

3. MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

(i) Wizi

(ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro.

(iii)Kugoma na kuhamasisha mgomo.

(iv)Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.

(v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule.

(vi)Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni. Aidha, kunyoa nywele kwa mtindo wa upara au mtindo wowote, mf."Kiduku, Bwenzi, Ngazi tatu" n.k .

(vii) Kufuga ndevu

(viii) Ulevi, matumizi ya madawa ya kulevya.

(ix)Uvutaji wa sigara au bange.

(x) Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.

(xi)Kupata ujauzito au kutoa mimba.

(xii) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi.

(xiii) Kusababisha au kumpa mimba msichana.

(xiv) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni (guest house)

(xv) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule.

(xvi) Kudharau bendera ya Taifa.

(xvii) (xvii)Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.

(xviii) Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi

4. **VIABATANISHO NA FOMU MUHIMU.**

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA OFISI YA RAIS - TAMISEMI.

SHULE YA SEC. MUBABA
S.L.P 185,
BIHARAMULO
TAREHE……

FOMUA.

MGANGA MKUU WAMKOA, WILAYA/ZAHANATI.

Jina ……. Amechaguliwa kujiunga na kidato cha ……. katika shule hii ili kuendelea na masomo ni lazima apimwe kwanza.

Nitafurahi iwapo mbali na kupimwa kijana huyu ataangaliwa uwezo wa kuona wa macho yake.

Kama imeshauriwa avae miwani hana budi kuinunua yeye mwenyewe kwa fedha zake.

Tafadhali nijazie sehemu inayohusika chini baada ya kumpima.

Ahsante kwa ushirikiano

……..

MKUU WA SHULE,

MKUU WA SHULE
MUBABA SHULE YA SEKONDARI
S.L.P 185,
BIHARAMULO.

Nimempima mwanafunzi aliyetajwa hapo juu na kuona kwamba ana matatizo/ugonjwa wa:-

A. Kifua kikuu……
B. Macho……
C. Masikio……..
D. Akili……...
E. Kilema chochote……
F. Choo (stool) ……..
G. Kwa wasichana tu nimeona ana/hana mimba ……
H. Mengineyo …….

SAINI NA MHURI WA OFISI…….

MGANGA MKUU WA MKOA/WILAYA/ZAHANATI.

FOMU B:

OFISI YA RAIS - TAMISEMI

SHULE YA SEKONDARI MUBABA

S.L.P 185, BIHARAMULO.

(A) MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI

Mimi……..

Naahidi kwamba sitashiriki mgomo wa aina yeyote wala kuchochea au kushawishi wengine kufanya mgomo wa aina yoyote kwa muda wote nitakaokuwa hapa shuleni.

Pia naahidi kwamba sitajiingiza katika makosa yoyote ya jinai ikiwa ni pamoja na ulevi, uvutaji sigara, Bangi na utumiaji wa madawa ya kulevya pia sitakuwa mtoro wa vipindi na utoro wa kudumu

Pia naahidi kuwa MTIIFU na kusoma kwa BIDII siku zote nikiwa mwanafunzi wa shule hii.

Jina …….. saini ……. Tarehe ……

(B) UTHIBITISHO WA MZAZI/MLEZI KUKIRI NA KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO MENGINE YANAYOTOLEWA NA SHULE.

Mimi …… ambaye ni MZAZI/MLEZI wa ……..

. . . . nimesoma na kuelewa sheria na taratibu za shule hii . Naahidi kuwa nitashirikiana na uongozi wa shule kuhakikisha kuwa mtoto wangu anafuata taratibu na miongozo yote itolewayo na shule kuhakikisha kuwa mtoto wangu anafuata taratibu miongozo yote itolewayo na shule kwa mujibu wa sheria na kanuni zilizowekwa mujibu wa sera ya Elimu ya Tanzania mwaka 2015.

Pia naahidi kuwa mtoto wangu atahudhuria masomo kwa muda wote kama inavyoelekezwa katika miongozo na sera ya Elimu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Jina……Saini……Tarehe……

……

MKUU WA SHULE

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII.

……...

Saini ya Mkuu wa shule

……

Jina la Mkuu wa Shule

……

Mhuri wa Mkuu wa s hule